# Mkulima Mbunifu

Jarida la kilimo endelevu Afrika Mashariki

biovision

Toleo la 70, Julai 2018


Yaliyomo


Faida za matandazo 3

Magonjwa ya mbuzi 4 & 5



Kilimo cha papai 6


## Vuna na uhifadhi malisho asilia kwa matumizi ya baadae




*Wafugaji wakiwa na mabelo ya nyasi za malisho*

Katika suala la ufugaji, malisho kwa ajili ya wanyama wafugwao linachukua sehemu kubwa sana. Hii ni kwa sababu malisho ndiyo nguzo kuu ya ustawi wa mifugo.

Pamoja na hayo, wafugaji walio wengi hawazingatii na kuweka mipango thabiti kwa ajili ya uvunaji na uhifadhi wa malisho kwa matumizi ya baadae.

Jambo hili ni hatari kwani inapotokea uhaba wa malisho, wafugaji huteseka kutafuta malisho, hali kadhalika huwatesa mifugo kwa kutokupata chakula cha kutosha.

Katika toleo hili tumekuandalia makala inayoeleza namna unavyoweza kuvuna malisho asilia na kuyahifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadae.

## Magonjwa yanayosumbua nguruwe na tiba zake

Nguruwe ni moja ya mifugo ambayo imejipatia umaarufu sana miongoni mwa jamii ya wafugaji nchini Tanzania kwa siku za karibuni. Hii ni kwa sababu nyama yake ina soko




*Nguruwe wenye afya*

kubwa hasa maeneo ya mijini, huku ikiwa na kundi kubwa la walaji, hivyo kusaidia wafugaji kuwa na pato zuri.

Pamoja na hayo, magonjwa husababisha hasara kwa mfugaji.


*Zaidi soma UK 2*


### MkM kwenye mtandao

Njia ya mtandao yaani internet, inawasaidia wale wote ambao hawana namna ya kupata machapisho ya Mkulima Mbunifu moja kwa moja, kusoma kwenye mtandao na hata kupakua nakala zao wao wenyewe.

mkulimambunifu.org
http://issuu.com/mkulimambunifu

http://www.facebook.com/mkulimambunifu

https://twitter.com/mkulimambunifu

+255 785 496 036

## *Mpendwa mkulima*

*Imekuwa ni jambo la kawaida kwa wakulima walio wengi kulalamikia kiwango cha uzalishaji katika mashamba yao, pamoja na kazi ngumu wanazofanya shambani kwa ajili ya uzalishaji.*

*Hali hii imekuwa ikikatisha wengi tamaa na nia ya kufanya shughuli za kilimo, ingawa kwa asilimia kubwa ya watanzania waliopo vijijini na mijini wanategemea kilimo.*

*Si hilo tu bali kilimo ndilo eneo linalotoa ajira ya uhakika kwa watu wote, kwani asilimia kubwa ya mahitaji yanategemea kilimo. Kila siku tunakula na kunywa kutokana na kilimo, kuvaa kilimo, na mengine kadha wa kadha.*

*Tatizo kubwa linalojitokeza hapa na kusababisha kuwa na uzalishaji duni unaosababisha malalamiko, ni kutokufuata taratibu inavyopaswa na kutokufanya kilimo salama ikiwa ni pamoja na matunzo duni ya udongo.*

*Ili mimea iwe na afya njema na kuweza kuzalisha ni lazima udongo uwe umetunzwa na kuwa na rutuba inayoweza kuneemesha mimea.*

*Pamoja na utunzaji wa udongo, wakulima pia wanahitaji kuwa na afya njema ili waweze kufanya kazi kwa uthabiti katika mashamba yao.*

*Mambo yote hayo ya kuwa na udongo wenye afya, wakulima kuwa na siha njema, na kuwa na uzalishaji thabiti, yanawezekana pale tu ambapo wakulima watafuata na kutumia njia za kilimo hai, ili kuepuka uharibifu wa udongo na afya zao kwa matumizi ya kemikali.*

*Ni dhahiri kuwa matumizi ya kemikali yanaua udongo kwani huharibu muundo wa udongo, na viumbe hai waliomo ardhini.*

*Mojawapo ya njia za asili zinazoweza kutumika katika uzalishaji wa mazao, zimeelezwa katika Makala iliyopo ukurasa wa tatu(3) na wa saba(7). Katika toleo hili.*


**MkM,** S.L.P 14402, Arusha, ***Simu*** 0717 266 007, 0785 133 005 ***Barua pepe*** info@mkulimambunifu.org, www.mkulimambunifu.org

# Fahamu baadhi ya magonjwa ya nguruwe na namna ya kukabiliana nayo

*Nguruwe ni moja ya mifugo ambayo imejipatia umaarufu sana miongoni mwa jamii ya wafugaji nchini Tanzania kwa siku za karibuni. Hii ni kwa sababu nyama yake, ina soko kubwa hasa maeneo ya mijini ,huku ikiwa na kundi kubwa la walaji, hivyo kusaidia wafugaji kuwa na pato zuri.*

**Amani Msuya**

Mfugaji anatakiwa kuzingatia afya ya mnyama ili pato liweze kuwa la kuridhisha. Hapa Tanzania magonjwa yanayosumbua nguruwe sio mengi, lakini hutokea mara kwa mara kufuatana na umri, mazingira na afya ya mnyama.

Magonjwa husababisha hasara kwa mfugaji kwani huweza kusababisha vifo, kupunguza uzito, ukosefu wa damu hasa kwa watoto na nguruwe kudumaa.



*Nguruwe wasipo tunzwa na kutibiwa mapema ni rahisi kufa na kusababishahasara*

Hivyo ni vizuri kuyazuia na kutoa taarifa kwa mtaalamu wa mifugo mara uonapo afya ya mnyama inabadilika. lakini visiweze kunyonywa na mimea.

**Yafuatayo ni baadhi ya magonjwa yanayoshambulia nguruwe hapa nchini.**

| *Ugonjwa* | *Husababishwa na* | *Dalili za Ugonjwa* | *Kinga na Tiba* |
|---|---|---|---|
| **Homa ya Nguruwe** *(African Swine Fever)* | Virusi<br>Huenezwa na Virusi<br>· Nguruwe wagonjwa kuchang-anyika na wasio wagonjwa<br>· Kula chakula chenye virusi<br>· Kupe laini | · Homa kali (41°C)<br>· Kuhema sana<br>· Kushindwa kala na kutembea<br>· Rangi ya ngozi hugeuka kuwa bluu au nyekundu<br>· Kifo baada ya siku 7.<br>· Kuharisha<br>· Huenea kwa kasi baada ya kutokea. | · Hakuna Tiba wala chanjo<br>· Nunua nguruwe kwenye mashamba yasiyo na historia ya ugonjwa<br>· Usafi wa vifaa, banda na mazingira yake<br>· Nunua vyakula vilivyothibitishwa<br>· Usitumie masalia toka sehemu zenye ogonjwa<br>· Tumia dawa za kuua kupe.<br>· Nguruwe wagonjwa wachinjwe. |
| **Ugonjwa wa Ngozi** | · Ukosefu wa vitamini<br>· Huenezwa na Viroboto, Chawa, Inzi na Utitiri | · Kujikuna mara kwa mara.<br>· Uvimbe kwenye ngozi.<br>· Hushindwa kula vizuri<br>· Hupungua uzito · | Ogesha nguruwe vizuri.<br>· Tumia dawa ya kuua viroboto, chawa, Inzi na utitiri<br>· Lisha nguruwe chakula chenye vitamini na madini ya kutosha. |
| **Kichomi** *(Pneumonia)* | Bakteria | · Homakali<br>· Kupumua harakaharaka na kwa nguvu<br>· Kikohozi kikavu | · Hakuna tiba<br>· Kiua bakteria hutumika kuzuia nmyama kush-ambuliwa na magonjwa mengine.<br>· Kuwatenga wanyama.<br>· Nyumba iwe na hewa na joto la kutosha. |
| **Midomo na Miguu** | Virusi<br>·Huenea kwa kugusana mnyama mgonjwa na mzima au kula chakula chenye virusi | ·Huwa na malengelenge miguuni, kwenye kiwele, midomoni na kooni.<br>· Hushindwa kula na kutem-bea. | · Hakuna tiba<br>· Apewe ohanjo<br>· Asipewe chakula chenye virusi<br>· Tibu Vidonda<br>· Karantini ya sehemu yenye ugonjwa. |
| **Kimeta** *(Anthrax)* | Bakteria | · Uvimbe kwenye mgongo<br>· Kupumua kwa tabu.<br>· Kifo cha ghafla<br>· Damu isiyoganda hutoka katika sehemu zilizo wazi | kama mdomoni, masikioni na puani.<br>· Apewe chanjo<br>· Nguruwe mgonjwa asichinjwe na aliyekufa asipasuliwe |

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa kila mwezi na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni moja wapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linasambazwa kwa wakulima bila malipo.

*Mkulima Mbunifu* linafadhiliwa na Biovision - www.biovision.

**Wachapishaji** African Insect Science for Food and Health (icipe), S.L.P 30772 - 00100 Nairobi, KENYA, Simu +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

**Mpangilio** Ibrahim Isack, +255 676 293 261 Zenith Media Ltd
**Mhariri Msaidizi** Flora Laanyuni
**Mhariri** Ayubu S. Nnko
**Mhariri Mkuu** Venter Mwongera
**Anuani** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction block) S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
**Ujumbe Mfupi Pekee**: 0785 496 036, 0766 841 366
**Piga Simu** 0717 266 007, 0785 133 005
**Barua pepe** info@mkulimambunifu.org, www.mkulimambunifu.org

# Fahamu vyanzo vya matandazo kwa ajili ya kilimo

*Matandazo kwa ajili ya kilimo hai hutokana na njia mbalimbali kama vile mazao funikizi, mabaki ya mazao, majani kutoka katika miti au vichaka na katika mimea mbalimbali.*

***Patrick Jonathan***



*Nyasi na mabaki ya mazao yanaweza kutumika kama matandazo*

Ikiwa matandazo yanategemewa kupatikana katika mazao funikizi, basi maandalizi ya eneo la kuoteshea na kukuzia mazao hayo ni lazima ufanyike.

**Matandazo kutoka katika mazao funikizi**

Baadhi ya mazao funikizi huzalisha na kuacha utando mwembamba wenye mabaki ya mimea hai na iliyokufa juu ya uso wa ardhi.

Kabla ya kuotesha zao jipya ni lazima kusafisha na kung'oa mimea hii. Kwa kufanya hivyo itasaidia kuzuia ushindani wa virutubisho kati yake na zao utakaloliotesha.

Pia unaweza kuondoa mimea hii kwa kufyeka, kung'oa mashina kwa kutumia majembe ya kukokotwa na wanyama, kazi na vifaa kama vile trekta na baadaye kuyatandaza juu ya uso wa ardhi kisha kuotesha zao jipya juu ya matandazo hayo.

**Matandazo kutoka katika mabaki ya mazao**

Mazao mbalimbali yanayooteshwa kwa msimu kama vile mahindi ni chanzo kikubwa cha matandazo mara baada ya kuvuna.

Unachotakiwa kufanya ni kuvuna kwa kukata mabua, kisha kuyalaza chini kufunika udongo na ikiwa hukuotesha mazao funikizi mabua haya yanatosha kuwa chanzo kizuri cha kurutubisha udongo.

Katika maeneo ambayo ni kame na hayana maji ya kutosha kuotesha mazao funikizi hasa kipindi cha kiangazi.

Njia ya kuacha mabaki ya mazao mara baada ya kuvuna kama matandazo ndiyo pekee inayofaa katika maeneo haya.

Wakulima katika maeneo mbalimbali huondoa kabisa mabaki ya mazao baada ya kuvuna. Hii ni kwa ajili ya kulishia mifugo na wakati mwingine huruhusu mifugo kuingia shambani kwa ajili ya kujilisha masalia hayo jambo ambalo husababisha uharibifu katika ardhi.

**Namna ya kuzuia uharibifu wa ardhi**

Mara baada ya kuvuna, jitahidi kuacha mabaki mengi ya mazao shambani. Mabaki hayo ni kwa ajili ya kutumika kama matandazo.

Ikiwa utahitaji kwa ajili ya kulisha mifugo, chukua kiasi kidogo tu cha mabaki yenye ubora na acha mengine kwa ajili ya kufunika uso wa ardhi.

Zuia uchungaji wa mifugo katika shamba, ili kusaidia kutokuharibu rutuba ya udongo pamoja na kuzuia kula mabaki yote ya mazao.

Tumia vyanzo vingine vya ulishaji wa mifugo kama vile kujitengea eneo maalumu kwa ajili ya kuotesha majani na kulisha mifugo yako.



*Mazao funikizi hasa jamii ya mikunde inasaidia sana kutunza udongo*

**Matandazo kutoka kwenye miti na vichaka**

Miti na vichaka hutoa majani mengi ambayo huweza kutumika kama matandazo katika kilimo na wakati huo huo, huweza kutumika kwa ajili ya kulishia mifugo.

Wakulima wanaweza kuona ni miti au vichaka gani wanaweza kupata matandazo kwa ya kilimo na kufunika udongo.

Kuna aina mbalimbali ya miti na vichaka vyenye kutoa matandazo yanayofaa kama yafuatayo;

**Miti yenye matumizi mbalimbali;** Baadhi ya miti huwa na matumizi mbalimbali kama vile kuzalisha mbao, matunda, lishe kwa wanyama na hata malazi.

Katika aina hii ya miti, mkulima anaweza kupunguza matawi au majani yake na kusambaza katika shamba lake kama matandazo.

**Miti ya fensi;** Miti hii huoteshwa kwa ajili ya kuweka uzio na ambayo mara nyingine hutumika kama malisho ya mifugo. Wakati huohuo huweza kupunguzwa na kutumika kama matandazo.

**Vichaka jamii ya mikunde;** Vichaka jamii ya mikunde kama vile gliricidia hutengeneza rutuba kwa kuongeza naitrojeni katika udongo. Unaweza kupanda kwa mzunguko wa mahindi au mtama kisha kukata na kutumia katika matandazo.

# Magonjwa ya kuhara pamoja na sumu

*Katika toleo lililopita, tuliangazia kwa undani juu ya magonjwa mbalimbali yanayoweza kuathiri mbuzi na namna ya kukinga. Tuliangazia magonjwa kama vile Ugonjwa wa viungo, kuugua kitovu na viungo, ugonjwa wa ngozi, homa ya maziwa, kuvimba kwa kizazi, na kutoka nje kizazi.*

**Flora Laanyuni**

Katika toleo hili tunahitimisha kwa kuangalia baadhi ya magonjwa ya kuhara na sumu mbalimbali ambazo mfugaji anatakiwa kujua ili kuwakinga mbuzi wasidhoofike au hata kufa.

**Magonjwa ya kuhara ni kama haya;**

1. **Ugonjwa wa kuhara *(Johne's disease)***

Ugonjwa huu husababishwa na bakteria ambao huchukuliwa ardhini. Aidha watoto wa mbuzi hupata ugonjwa huu kwa njia ya kunyonya maziwa yenye bakteria.

Huu ni ugonjwa sugu unaowapata mbuzi wenye umri wa miaka 2 hadi 5.

Mbuzi huweza kuwa katika hali ya kukosa raha na muda mfupi tu mara baada ya kuzaa, hivyo unaweza kufanya kuanza kujionyesha.

**Dalili**

Mbuzi huharisha, hukonda taratibu kutokana na bakteria kuingilia mfumo wa ufyonzaji wa viinilishe kuingia mwilini na utoaji wa maziwa kupungua.

**Jinsi ya kuzuia**

Kwa kuwa ugonjwa huu hauna tiba, mbuzi watakaokuwa wameambukizwa wachinjwe.

Aidha, mbuzi wanaoingizwa nchini wafanyiwe uchunguzi wa kina kuhakikisha kuwa hawana ugonjwa huu kabla ya kuletwa.

2. **Ugonjwa wa kuhara *(Salmonellosis)***

Ugonjwa huu wa kuhara kwa mbuzi husababishwa na bakteria aina ya *Salmonella.*

**Dalili**

Mbuzi huwa na dalili ya kuharisha kinyesi cha majimaji. Kinyesi huwa na rangi ya njano kuelekea kijani cha kahawia. Huwa na harufu mbaya sana na mbuzi mwenye mimba, huweza kutupa mimba.

**Tiba**

Mbuzi mwenye ugonjwa huu, atibiwe kwa antibaiotiki kama vile Tetracycline au Sulpha.

**Jinsi ya kuzuia**

Banda la mbuzi lililochafuliwa kwa kinyesi, lisafishwe kwa dawa za kuangamiza vijidudu.

3. **Ugonjwa wa kuhara *(Calibacillosis)***

Ugonjwa huu huathiri zaidi watoto wa mbuzi na husababishwa na bakteria wajulikanao kama Escherichia colli.

**Dalili**

Watoto wa mbuzi huharisha kinyesi cha majimaji, midomo yao kukauka na tumbo kujaa hewa.

Mtoto wa mbuzi anayeugua ugonjwa huu huishiwa maji haraka, na hufa iwapo hatapata huduma inayostahili.

**Tiba**

Mbuzi anyweshwe mchanganyiko wa maji safi yenye chumvi na sukari, au chumvi maalumu kwa ajili ya wanyama wanaoharisha *(Oral rehydration salt).*



*Mbuzi wanaweza kupata magonjwa kutokana na sehemu wanapolishwa*


*Mbuzi wanahitaji matunzo*

Mbuzi pia wanaweza kutibiwa kwa kudungwa sindano au kwa kunyweshwa dawa ya antibayotiki.

**Jinsi ya kuzuia**

Hakikisha watoto wa mbuzi wanapata maziwa ya mwanzo, yaani dang'a *(colostrum)*, mara tu baada ya kuzaliwa na kisha kutunzwa katika mazingira safi.

4. **Ugonjwa wa kuhara *(Coccidiosis)***

Ugonjwa huu wa kuharisha mara nyingi mbuzi hutoa kinyesi chenye damu na mbuzi huweza kupoteza uzito kwa haraka sana.

**Tiba**

Mbuzi wenye ugonjwa huu watibiwe kwa Sulpha au Amprolium.

**Jinsi ya kutibu**

Ili kuweza kutibu ugonjwa huu, mfugahi hana budi kuzingatia usafi. Watoto wa mbuzi wawekwe mahali pakavu na wasirundikwe mahali padogo.

**Sumu zinazoweza kuathiri mbuzi**

Pamoja na kuwa kuna magonjwa mengi yanayoweza kuathiri mbuzi, pia sumu zinazopatikana katika baadhi ya miti, mimea, dawa au

# zinazoweza kuathiri mbuzi



bora ili kuepuka magonjwa

hata wanyama, huweza kusababisha mbuzi kufa mara atakapokula.

Baadhi ya sumu zinazoweza kusababisha mbuzi kufa ni kama zifuatayo;

**a. Sumu ya lukina**

Mmea huu una sumu iitwayo mimosine, ambayo ikiliwa kwa kiasi kikubwa huleta madhara kwa mbuzi.

**Dalili**

Mbuzi aliyekula sumu hii ngozi yake hujenga mabaka ya utando ambao baadaye hubanduka.

**Jinsi ya kuzuia**

Hakikisha mbuzi hali kiwango cha lukina kinachozidi 1/3 ya malisho yote anayolishwa kwa siku.

**b. Sumu ya *lantana camara***

Mmea huu haupendwi na mbuzi, lakini mara nyingi mbuzi wakiwa na njaa kali hula. Hali hii hutokea wakati wa ukame, ambapo malisho huadimika kwa kiasi kikubwa.

Mbuzi akila kiasi kikubwa cha mmea huu hudhurika sehemu za kichwani na masikio.

**Dalili**

Mwanga wa jua humuumiza mbuzi macho na kumfanya auogope mwanga huo na mara nyingi kukaa kivulini au kuligeuzia jua mgongo. Sehemu nyeupe au zenye rangi hafifu zinazopigwa na jua hupata vidonda na mbuzi huweza kuharisha sana.

**Tiba**

Mbuzi atunzwe mahali penye kivuli na vidonda vitibiwe kwa kutumia Sulfanilamide ya unga. Tumia dawa ya kufukuzia inzi kama kutakuwa na haja.

**Jinsi ya kuzuia**

Mbuzi wasilishwe mimea hii na kama ni lazima walishwe basi wapewe kiwango kidogo sana.

**c. Sumu ya mmbono**

Sumu iitwayo ricin hupatikana zaidi kwenye mbegu na vilevile kenye majani na shina la mmbono.

**Dalili**

Mbuzi akila sumu hii hutapika, hupata kiu sana, huharisha na uyeyushaji wa chakula tumboni husimama na hatimaye mbuzi hufa.

**Jinsi ya kuzuia**

Namna ya kuzuia sumu hii ni moja tu, hakikisha mbuzi hawali mmea huu.

**d. Sumu ya ndulele**

Sumu ya glycoalkaloids inayopatikana kwenye matunda ya ndulele si nzuri kwa mbuzi japokuwa mbuzi huweza kula kwa nadra sana.

**Dalili**

Mbuzi aliyekula sumu hii hupata udhaifu na kuanza kutetemeka, kuvimbia au kuharisha na hatimaye kufa.

**Jinsi ya kuzuia**

Mbuzi wasiachwe bila kupewa malisho kwa muda mrefu na kisha kulishwa malisho yenye mchanganyiko wa mmea huu ili kuepuka kula sumu.

**e. Sumu ya dawa za kuogeshea**

Mbuzi akimeza sumu hii hutoa machozi na mate, huwa na mshtuko, hutoa jasho na huweza kufa ghafla.

**Tiba**

Ikigundulika kuwa mbuzi amekula sumu hii, basi atibiwe kwa kudungwa sindano ya *atropine sulphate.*

**Jinsi ya kuzuia**

Hakikisha dawa hizi zinawekwa mbali na mbuzi, hasa dawa za kuogeshea kama vile organophosphate.

**f. Sumu ya nyoka**

Mbuzi akiumwa na nyoka akiwa malishoni na kupata sumu ya nyoka humuathiri.

**Dalili**

Mbuzi huweza kupumua kwa shida, kuwa na mshtuko, kutoa mate na jasho na hata kufa kwa ghafla.

**Tiba**

Mbuzi apatiwe dawa ya sumu ya nyoka kama ameumwa mguu kwa kufunga kamba upande wa juu wa mguu ili kupunguza kuenea haraka kwa sumu mwilini.

Pia mbuzi anaweza kutibiwa kwa kupatiwa *antibaiyotiki na asteroid*.

**Jinsi ya kuzuia**

Epuka kulisha mbuzi kwenye mazingira ambayo yataongeza uwezekano wa mbuzi kuumwa na nyoka.

***Kwa maelezo Zaidi unaweza kuwasiliana na mtaalamu wa mifugo Fransic Ndumbaro kwa simu namba +255 754 511805***



*Mbuzi mwenye ugonjwa wa coccidiosis*

# Kilimo cha Papai: Ujasiriamali unaowakomboa wakulima

*Papai ni aina ya zao la matunda lenye asili ya ukanda wa kitropiki, ambao hauna baridi kali na joto la wastani.*

**Ayub Nnko**

Papai ni tunda lenye ladha nzuri, na rahisi kuliwa. Hii ni moja wapo ya matunda yenye virutubisho muhimu katika mwili wa binadamu, vinavyosaidia kujenga mwili.

**Maandalizi ya miche**

- Loweka mbegu za papai kwenye maji safi kwa siku tano na kila siku uyabadilishe maji asubuhi.
- Baada ya kuloweka siku tano, hamisha mbegu kwenye taulo bichi.Funika mbegu ndani ya taulo kwa siku tatu.
- Weka taulo sehemu ambayo hakunna mwanga.

**Maandalizi ya kitalu**

Andaa eneo linalofaa kwa ajili ya kuweka kitalu. Ni muhimu kuzingatia kanuni zinazoongoza utengenezaji wa vitalu. Kitalu cha miche ya papai uzingatie mambo yafuatayo:

- Udongo wa msituni ni bora kwa uaandaaji wa kitalu endapo utapatikana kirahisi.
- Endapo utakosa udongo wa msitu, chukua udongo wa kawaida.Changanya na mbolea ya wayama au mboji kwa resho ya 3:1. Mfano: Ndoo 3 za udongo, ndoo 1 ya mbolea ya samadi au mboji.
- Changanya udongo vizuri na uchanganye na maji mpaka uwe na unyevu kiasi flani.
- Weka kwenye viriba, acha kwa siku tatu huku ukimwagilia kila siku.
- Panda mbegu katika viriba.
- Toboa udongo kidogo kama sm1-2.Panda na kufunika mbegu kwa udongo.
- Mbegu zitaanza kuota katika kipindi cha Siku 4-6.
- Pima udongo kama haua unyevu wakuridhisha mwagilia.
- Miche ikiwa na 15cm-20cm itakuwa tayari kwenda shambani.

**Uandaaji wa shamba**

Inashauriwa kuandaa shamba vizuri kwa kuondoa visiki na magugu yote. Shamba lilimwe vizuri, na kuhakikisha udongo umelainika vizuri.

**Maandalizi ya mashimo**



Kilimo cha papai hakina ghalama kubwa ila uzalishaji mkubwa

Ili kuwa na matokeo mazuri, ni muhimu sana kuzingatia vipimo na nafasi sahihi upandaji wa papai.

Nafasi Kutoka Shimo na Shimo

1. 2m X 2m Mstari kwa mstari.
2. 2mx2 Shina kwa Shina.

**Maandalizi ya mashimo**

- Chimba shimo lenye Urefu-60sm, Upana-60sm, Kimo-60sm
- Baada yakuchimba mwagilia shimo hilo.
- Rudisha mchanganyiko wa udongo na samadi ndani ya shimo.
- Baada yakurudishia udongo acha kwa wiki mbili, huku ukimwagilia shimo ili kupooza mbolea.
- Wakati huo miche iwe sehemu salama, ukiwa una mwagilia kwa siku tatu. Hii itasaidia mche kuzoea mazingira.Baada ya siku tatu, kata plastiki iliyo funika udongo wa mche taratibu.
- Panda mche wa papai na hakikisha udongo haupukutiki.

**Matandazo**

Matandazo ni majani au mabaki ya mazao shambani, yanayo wekwa chini ya mmea ili kuhifadhi unyevunyevu kwa muda mrefu na kuupa mmea uwezo wakuchukua maji kidogodogo na kuzuia wadudu pamoja na magugu.

Baada yakupanda mche wa papai hakikisha unaweka matandazo kuzungaka mmea/papai

**Mbolea**

- Epuka matumizi ya mbolea za viwandani, hasa zenye chlorine. Hii ni kwa sababu papai huathiriwa na chlorine kwa kiasi kikubwa.
- Wiki moja baada ya kuhamisha miche yako tumia mbolea mboji iliyoiva vizuri kiasi cha gramu 28 kwa mmea.
- Baada ya hapo kila baada ya wiki mbili weka mbolea yenye Naitrojeni kwa kiasi kikubwa cha gram 56 kwa mmea.
- Potashiamu inahitajika kwa maua na kuweka matunda.
- Tumia mbolea yenye potashiamu kiasi kikubwa mara baada ya kuona mmea wako umeanza kuweka maua. Fanya hivyo kila baada ya mwezi.
- Weka mbolea ya majani yenye virutubisho vidogo vidogo ikiwemo Boron kila mwezi.
- Boron ni mbolea muhimu katika kupata matunda muzuri.
- Kila mwaka hakikisha unaweka mbolea mboji debe moja, kwa kuchimbia pembeni na kufunika.

**Umwagiliaji**

Maji ni muhimu sana katika maisha ya mmea kwa kipindi chote. Maji ni muhimu katika kuweka maua, matunda na ukuaji wa matunda.

Inaendelea UK 8

# Uvunaji na uhifadhi wa malisho asilia kwa mifugo

*Mfugaji ambaye hajaweza kuchagua eneo na kulitunza kwa ajili ya baadae kukata nyasi, anaweza kutafuta eneo la kuvuna malisho ya mifugo*

*SAT*



Wafugaji wakitengeneza belo la nyasi za malisho

Malisho asilia ni uoto unaoota katika mazingira ambayo hayajaandaliwa rasmi kwa upandaji wa mbegu., zaidi tu ya usimamizi na kuzuia uvamizi wa mifugo kwenye eneo hilo wakati wa uotaji na ukuaji wake.

**Uchaguzi wa eneo**

Chagua eneo lenye nyasi nzuri na kiwango kikubwa cha malisho, usiruhusu uchungaji wa mifugo katika eneo hilo. Eneo hilo linaweza kurutubishwa kwa kuweka/ kusambaza samadi ili kuongeza virutubisho kwenye udongo, hivyo kupata nyasi bora na zilizokua vizuri.

Kwa mfugaji ambaye hajaweza kuchagua eneo na kulitunza kwa ajili ya baadae kukata nyasi, anaweza kutafuta eneo la kuvuna malisho ya mifugo kwa kuzungukia maeneo yote yenye majani na kuchagua majani yanayofaa.

**Aina ya majani yanayofaa kuchaguliwa kwa malisho**

Majani jamii ya nyasi yasiyo na asili ya ugumu yakikauka, na yasiyo na kijimti kikubwa au kirefu ndio bora kwa mifugo. Mfano wa majani yanayofaa ni nyasi jamii ya Mbudu, na mengineyo ya aina hiyo.

**Wakati wa uvunaji**

Ili kupata malisho bora ya mifugo nyasi zinatakiwa kuvunwa wakati wa ukuaji (siku chache kabla ya kuanza kutoa maua). Huu ni wakati ambao malisho yanakuwa na virutubisho muhimu kwa afya na ukuaji wa mifugo.

Nyasi zinapoanza kutoa maua virutubisho vingi hupotea, hivyo inatakiwa uanze kuvuna kabla hayajaanza kutoa maua. Kwa mfugaji aliyechelewa kuandaa na kutafuta eneo la kuvuna malisho, avune wakati wowote ila ahakikishe malisho hayajakauka yenyewe kabla ya kukatwa.

**Vifaa vya kukatia nyasi**

Kuna vifaa vinavyotumika katika uvunaji wa malisho asilia kulingana na uwezo wa mfugaji mwenyewe. Vifaa vinavyotumika ni mundu uliopindwa (Sickle) kwa ajili ya kukata nyasi, kisu kwa ajili ya kukata kamba ya kufunga majani na panga kwa ajili ya kuondoa vichaka kabla ya kukata majani.

**Ukaushaji**

Malisho hukatwa na kuachwa juani kwa muda wa siku mbili, baada ya hapo huwekwa kivulini chini ya mti tayari kwa ajili ya utengenezaji wa marobota(belo).

**Ubora wa malisho yaliyokaushwa**

Malisho yaliyokaushwa vizuri hayana fangasi. Dalili za kuharibika kwa nyasi ni pamoja na kuwa na fangasi wa rangi ya kijivu, kijani au nyeusi. Majani yakiwa katika hali hii hayatakiwi katika malisho. Fangasi husababisha madhara mbalimbali ikiwamo mifugo kujaa matumbo.

**Ufungaji wa malisho yaliyokaushwa**

Kifaa kinachotumika kwa ajili ya malisho yaliyokaushwa ni boksi lenye ukubwa wa urefu inchi 30, upana inchi 17 na kina cha boksi inchi 10.5. Boksi linatakiwa kuwa na uwezo wa kukunjuka katika pembe/kona tatu ili kurahisisha utoaji wa balo la nyasi zilizokaushwa.

**Namna ya kufunga**

Utatakiwa kukunja boksi na kutengeneza mstatili, huku komeo lake likiwa imefungwa vizuri. Baada ya hapo, jaza nyasi ndani ya boksi na shindilia vizuri kwa kutumia miguu ukiwa umevaa kiatu kisafi.

Balo moja lililojazwa na kushindiliwa vizuri inaweza kuwa na uzito wa kilo 15 na kuendelea kufuatana na aina ya nyasi, ukaushaji na ushindiliaji mzuri.

**Namna ya uhifadhi wa malisho yaliyokaushwa**

Malisho huhifadhiwa kwenye eneo ambalo hakuna jua la moja kwa moja, mbali na mvua ili kutunza ubora wake. Matumizi ya kichanja ni muhimu kwa sababu nyasi haitakiwi kuwekwa juu ya ardhi/sakafu ili kutoruhusu uotaji wa fangasi na kusababisha kuharibika kwa malisho.

Malisho yaliyokaushwa huweza kuhifadhiwa kwa zaidi ya miaka mitatu kama yamehifadhiwa vizuri, mbali na unyevu pia sehemu inayopitisha hewa ya kutosha wakati wote.

**Ulishaji**

Malisho yaliyokaushwa hulishwa kwa kufungua kamba, kutoa nyasi na kumpatia ng'ombe au mifugo mingine. Belo moja linaweza kukidhi mahitaji ya ng'ombe mmoja au zaidi kwa siku kulingana na ukubwa wa ng'ombe.

Kwa nyasi zilizokaushwa hula wastani wa asilimia 3 hadi 5 ya uzito wa mwili wake, pia atatakiwa kunywa maji lita 10 hadi 15 baada ya kula.

***Makala hii imeandaliwa na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT).***

Inatoka Uk.6

# Kilimo cha Papai: Ujasiriamali unaowakomboa wakulima

Wakati wa ukuaji wa matunda hakikisha unaweka lita 23 kwa kila mmea kwa wiki. Kwa wastani wa lita tatu (3) za maji kila siku.

Umwagiliaji utakuwa wa ufanisi iwapo utakuwa wa matone na kuweka matandazo kwenye mashina.

**Magugu**

Magugu ya dhibitiwe kipindi cha mwanzo ili kuzuia ushindani kati ya mmea na magugu kwa virutubisho na maji. Pia kuzuia kubeba wadudu na magojwa wanao weza kuathiri uzalishaji wa papai.

**Hatua za ukuaji wa papai**

1. Kitalu-wiki 1-6
2. Hatua ya ukuwaji wa haraka baada ya kuhamishiwa shamba –wiki 7-16
3. Maua na kuweka matunda –wiki 17-21
4. Kukua kwa matunda –wiki 22-26
5. Mavuno ya kwanza –wiki 37 nakuendelea



Picha: MkM

*Mipapai inahitaji matunzo thabiti kwa uzalishaji bora*

Wakulima wanaozingatia kanuni za kilimo bora huzalisha mapapai zaidi ya 40 kila Mpapai kwa mwaka.

***Kwa maelezo Zaidi unaweza kuwasiliana na Mosses Anney +255752972727, Barua Pepe: mosesanney@gmail.com Web: www.formalagro.blogspot.com***

# Natumia mkojo wa Sungura katika kilimo cha Papai

"Napenda sana kilimo cha papai, na napenda kuzalisha mazao yote kwa misingi ya kilimo hai. Ndiyo sababu niliamua kufuga sungura nipate mkojo wake kwa kuwa una virutubisho vingi kwa mazao"

Ndivyo alivyoanza kueleza Lena Hulda Kileo(74) mkazi wa kijiji cha Kilingi, Wilaya ya Siha, alipotembelewa na MkM Shambani mwake.

Bi. Lena kileo ni mmoja wa wakulima wa Papai wanazalisha kwa kufuata misingi ya kilimo hai wilayani humo.



Picha: MkM

*Bibi Lena Hulda Kileo mkulima wa papai*

**Ni kwa nini anapenda kilimo cha Papai?**

- Lena anatanabaisha kuwa mipapai inachukua eneo dogo.
- Uzalishaji mkubwa kwa gharama ndogo.
- Mavuno ya muda mrefu.
- Hahitaji nguvu kazi kubwa.
- Hakuna usumbufu wa ufuatiliaji kwa karibu kama ilivyo mazao mengine.

**Kwa nini kutumia mkojo wa Sungura?**

Lena anaeleza kuwa anapenda kutumia mkojo wa sungura shambani mwake kwani una virutubisho vingi vinavyowezesha mazao yake, hasa mipapai kustawi vizuri.

Pia mkojo wa Sungura hutumika kama kiuatilifu na kuzuia wadudu wa aina mbalimbali kuingi katika mazao.

Huku akionesha mipapai alikotumia mkojo wa Sungura anaeleza kuwa kijani kwenye majani ni tofauti sana na eneo ambalo mkojo wa sungura haukutumika.

**Matarajio**

Bibi Lena anatarajia kuongeza kipato kutokana na mauzo ya papai, ambapo katika eneo la robo heka, anatarajia kupata kiasi cha shilingi milioni tisa mpaka kumi na moja.

**Changamoto**

Lena anaeleza kuwa kilimo cha papai si cha asili yake, ni cha kujifunza hivyo inapotokea tatizo inakuwa vigumu kutatua kwa haraka mpaka atafute wataalamu.

Mabadiliko ya hali ya hewa kama vile wingi wa mvua unaathiri uzalishaji inavyotakiwa.

**Ushauri**

Ni muhimu sana kufanya utafiti kabla ya kuanza shughuli fulani. Si vyema kufanya mambo kwa kuiga bila kuwa na uhakika.

***Unaweza kuwasiliana na Lena Kileo kwa namba +255754831353***